



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
OFISI YA RAIS**



**TAWALA LA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA WILAYA YA HAI  
(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi Mtendaji)**

**MKOA WA KILIMANJARO**

Simu : 27- 29 74369

Mtendaji Wilaya,

Fax : 27- 29 74368

Email: [ded@haidc.go.tz](mailto:ded@haidc.go.tz)

Kumb NA LG/ 2020/2021.

Ofisi ya Mkurugenzi

S.L.P. 27,

HAI.

Tarehe : 29/03/2022

**TANGAZO**

**TANGAZO LA KUMPATA FUNDI (LOCAL FUNDI) KWA  
AJILI YA UJENZI WA JENGO LA MAABARA KATIKA  
HOSPITALI YA WILAYA YA HAI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Hai kupitia Hospitali ya wilaya anategemea kuanza ujenzi wa jengo la Maabara katika Hospitali ya Wilaya ya Hai.

Hivyo napenda kuwatangazia mafundi wote (local fundi) wenye uwezo wa kujenga majengo ya serikali wajitokeze na kuomba kazi hii.

Mafundi wenye sifa na uzoefu wanatakiwa kuja kuchukua fomu maalumu (schedule of labour) dondoo shindani katika ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi Halmashauri ya Wilaya ya Hai.

**Sifa za Mwombaji.**

1. Awe ni raia wa Tanzania mwempe uelewa mzuri wa lugha ya Kiswahili na Kiingereza
2. Awe na umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea.
3. Awe na uelewa mzuri wa usalama na Afya awapo eneo la kazi.
4. Awe na timu ya kutosha ya mafundi mbalimbali kwa muda wote wa kazi mfano fundi mwashi, fundi bomba, fundi umeme, fundi carpenta nk.
5. Awe na uwezo wa kuandaa na kutekeleza mpango kazi wa mradi /miradi na kumaliza kwa wakati.
6. Awe mwadilifu na mwaminifu.
7. Uwezo wa kusimamia mafundi wenzake na vibarua.

8. Mwenye zana zote muhimu za kazi (tools).
9. Ada ya maombi ya kazi ya ufundi ni shilingi elfu ishirini (20,000/=) fedha hii haitarudishwa

### **Uzoefu.**

1. Uzoefu wa kuanzia miaka mitano na kuendelea katika kazi ya ujenzi.
2. Awe amefanya kazi yoyote ya ujenzi /ukarabati wa majengo ya serikali walau miradi mitatu na hati ya huduma (certificate of service) au mikataba ya miradi iliyotekelezwa ambayo inafikika kwa udhibitisho(ambatanisha udhibitisho).
3. Awe na uwezo wa kusoma na kutafsiri mchoro/michoro ya majengo kwa lugha ya kiufundi.

Maombi ya kazi hii zinapatikana ofisi ya Mkuu wa Kitengo cha manunuzi na ugavi na baada ya fomu kujazwa yawekwe katika bahasha iliyofungwa vizuri na kuandikwa anuani ifuatayo , Mkurugenzi Mtendaji  
Halmashauri ya Wilaya  
Hai.S.L.P 27 Hai.

Mwisho wa kupokea maombi haya ni 4:00 asubuh tarehe 05/04/2022 sehemu ya kuwasilisha maombi hayo ni ofisi ya Manunuzi na Ugavi Wilaya ya Hai S.L.P 27 . Ufunguzi wa maombi hayo utafanyika tarehe 05/03/2022 katika Ukumbi wa Halmashauri mbele ya waombaji watakaopenda kuhudhuria ufunguzi huo.

**ANGALIZO:** Fundi anatakiwa kujaza fomu ya ombi kwa kupitia mchoro wa jengo husika.

Limetolewa na



Rajabu Yateri  
Kaimu Mkurugenzi Mtendaji (W)  
**HALMASHAURI YA WILAYA-HAI.**

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)**  
**HAI**